

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26- 2323201-7  
Nukushi: +255-26-2323208  
Barua pepe: [nje@nje.go.tz](mailto:nje@nje.go.tz)  
Tovuti: [www.foreign.go.tz](http://www.foreign.go.tz)



Jengo la LAPF Ghorofa ya 6,  
Barabara ya Makole,  
S.L.P 2933,  
DODOMA.

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

#### SERIKALI YA BRAZIL IMETANGAZA RASMI KUFUNGUA MILANGO YA USHIRIKIANO WA KIFEDHA NA BIASHARA NA TANZANIA

Serikali ya Brazil imesamehe Tanzania deni la jumla ya Dola za Marekani milioni 203 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania zaidi ya Bilioni 445. Deni hilo lilitokana na mkopo uliotolewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Morogoro-Dodoma mwaka 1979 pamoja riba.

Hayo yamebainishwa kwenye hafla ya uwekaji saini wa mkataba huo wa msamaha ambapo Balozi wa Tanzania Nchini Brazil Dkt. Emmanuel Nchimbi amesaini mkataba huo kwa niaba ya Tanzania huku Wakili wa Hazina ya Taifa Dkt. Sonia Portella Nunes akisaini kwa niaba ya Serikali ya Brazil.

Balozi Nchimbi ameishukuru Serikali ya Brazil kwa Msamaha huo ambao amesema umeunga mkono jitihada za Rais Dkt. John Pombe Magufuli kujenga uchumi imara wa Tanzania.

Balozi Nchimbi pia ameihakikishia Serikali ya Brazil utayari wa Tanzania katika kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uchumi na Brazil.

Kwa upande wake, kiongozi wa ujumbe wa Brazil kwenye sherehe hiyo Bw. Guilheme Laux, Undersecretary of Credit and Guarantee kutoka Wizara ya Fedha ya Brazil alitamka rasmi kufunguliwa kwa milango ya ushirikiano wa kifedha na kibiashara iliyokuwa imefungwa kutokana na Deni hilo lililofanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye madeni sugu ya Brazil.

Hivyo kutoka sasa Makampuni ya Brazil yanaruhusiwa kukopa katika

Benki za Brazil kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na uwekezaji nchini Tanzania lakini pia Serikali ya Tanzania inaruhusiwa kuanzisha majadiliano ya miradi mipya ya maendeleo na Serikali ya Brazil.

**-Mwisho-**

**Imetolewa na:  
Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Brasilia, Brazil. Septemba 17, 2017**